



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA
UTEKELEZAJI WA MRADI WA SEQUIP 2021/2022
UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI UHAMAKA

KUANZIA TAREHE 01 FEBRUARI, 2022 HADI 14 MACHI, 2022

Halmashauri ya Manispaa ya Singida mwishoni mwa mwezi Desemba ilipokea fedha kiasi cha **Tshs. 470,000,000** kupitia Mradi wa SEQUIP kati ya Tshs. 600,000,000 zilizoombwa kwa ajili ya kuboresha Miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika shule za sekondari.

Akitoa maelezo ya Mradi huo Mkuu wa shule ya Sekondari Mandewa Ms. Goergia Maghiya, ambayo ni shule mama ya Sekondari ya Uhamaka amesema kulingana na muongozo uliotolewa, Mradi huo umeelekezwa katika kukamilisha ujenzi wa majengo ya shule ya sekondari ya Kata ya Uhamaka ambapo ujenzi huo utahusisha jengo la utawala, vyumba 08 vya madarasa vyumba 03 vya maabara, chumba 01 cha ICT, chumba kimoja cha maktaba, matundu 20 ya vyoo, tanki la kuvuna maji na mifumo ya kunawa mikono.

Hadi kufikia tarehe 14.03.2021 tayari kiasi cha **Tshs. 214,950,802.10** kimetumika katika utekeleza wa shughuli mbalimbali za Mradi huo ambao unatekelezwa kwa kutumika '**force account**' ambapo ili kuendana na muda Mradi umegawanywa kwa mafundi wanne (lot. 1,2,3&4) ambao walianza kazi ndani ya siku tatu baada ya kusaini maktaba wa kazi tarehe 01/02/2022

- Lot. 01 – ujenzi wavyumba 08 vya madarasa
- Lot. 02 – ujenzi wa jengo la utawala na chumba kimoja cha maktaba
- Lot.03 - ujenzi wa vyumba 03 vya maabara na chumba 01 cha ICT
- Lot. 04 – ujenzi wa matundu 20ya vyoo

Utekelezaji wa Mradi

Jina la Shule: Sekondari ya Kata ya Uhamaka

Mradi (Lot.1): Ujenzi wa vyumba 08 vya madarasa

Tarehe ya kuanza mradi: 01 Februari, 2022

Tarehe ya kumaliza Mradi: 30 Mei, 2022

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo hatua ya uezekaji. Mbao za kenchi zimepandishwa tayari kwa kupiga bati.



Mwonekano wa Vyumba 02 vya madarasa vikiwa hatua ya lenta. Vyumba vingine 06 pia viko katika hatua ya ufungaji lenta



Ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa ukiwa unaendelea katika hatua ya uezekaji



Zoezi la uwekaji kenchi katika vyumba 04 vya madarasa ukiendelea



Uwekaji kenchi katika vyumba 02 vya madarasa ukiendelea. Vyumba vyote 08 vya madarasa viko katika hatua ya upauzi tarehe 14.03.2022

Mradi (Lot. 2): Ujenzi wa jengo la utawala na chumba 01 cha maktaba

Tarehe ya kuanza mradi: 01 Februari, 2022

Tarehe ya kumaliza Mradi: 30 Mei, 2022

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo katika hatua ya upauzi.



Jengo la utawala likiwa katika hatua ya ukamilishaji wa hanamu tarehe 25/02/2022.



Jengo la utawala likiwa katika hatua ya upauzi tarehe 14.02.2022

Mradi (lot.3): Ujenzi wa vyumba 03 vya maabara na chumba 01 cha ICT

Tarehe ya kuanza mradi: 01 Februari, 2022

Tarehe ya kumaliza Mradi: 30 Mei, 2022

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo katika hatua ya uezekaji.



Ujenzi wa vyumba 03 vya maabara ukiwa katika hatua ya kufunga lenta tarehe 25.02.2022



Jengo la maabara likiwa katika hatua ya upauzi tarehe 14.03.2022

Mradi (lot , 04): Ujenzi wa matundu 20 ya vyoo

Tarehe ya kuanza mradi: 01 Januari, 2022

Tarehe ya kumaliza Mradi: 30 Aprili, 2022

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo katika hatua ya uezekaji



Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo vya wasichana ukiwa katika hatua ya kufunga lenta tarehe 25.02.2022



Mwonekano wa ubavuvi wa jengo la vyoo vya wavulana matundu 10 tarehe 25.02.2022



Ujenzi wa matundu 20 ya vyoo ukiwa katika hatua ya upauzi tarehe 14.03.2022